# TEKA

## Mafanikio yako

### Jinsi ya Kuifanya Dunia Kuwa Bora Zaidi ya Ulivyoikuta



**Jegi Nimuka Bassu**

# TEKA MAFANIKIO YAKO

**Jinsi ya Kuifanya Dunia Kuwa Bora Zaidi ya Ulivyoikuta**

**Jegi Nimuka Bassu**

Jegi Nimuka Bassu

**TEKA MAFANIKIO YAKO**

© 2022 Jegi Nimuka Bassu

Haki zote za kitabu hiki zimehifadhiwa. Huruhusiwi kunakili au kudurufu sehemu yoyote ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi na mchapaji. Ikigundulika hatua za kisheria zitachukuliwa.

**Mawasiliano na Mwandishi:**
Jegi Nimuka Bassu
Mbeya, Tanzania.
Simu +255 754 553 303
Barua pepe: iliketanz@gmail.com

Kimesanifiwa na Kupangwa na **Maige Gambishi**
Kigoma, Tanzania
+255 752 336 214
mygmoses@gmail.com

Cover Design: LD-Lamax Designs
Dar es Salaam, Tanzania
+255 764 793 105

## Shukrani

Shukrani za kwanza ziende kwa Mwenyezi Mungu Muumba wangu kwani bila yeye kuamua kuniumba na kunijaalia ujuzi na maarifa kazi hii isingewepo.

Shukrani za pili ni kwa wazazi wangu; baba yangu **Bassu Nimuka Shindai** (Mungu amuweke mahali pema peponi) na mama yangu **Maria Magomasi**. Juhudi zao za kutaka nisome ili nije kulitumikia Taifa letu la Tanzania na dunia kwa ujumla hakika zimezaa matunda.

Shukrani za pekee ziende kwa walimu wangu wote katika hatua mbalimbali za elimu nilizopitia; katika elimu rasmi na elimu nje ya shule. Mungu wetu awabariki sana.

Pia natoa shukrani kwa familia yangu, ndugu zangu, jamaa na marafiki. Bila wao na jitihada zao kuniimarisha naamini baadhi ya mambo niliyoyaandika humu nisingekuwa na ujasiri wa kuyaandika. Mungu aendelee kuwatia nguvu.

Bila kukusahau wewe unayesoma kitabu hiki, nakushukuru sana kwa kuwa naamini unanijali na kuzidi kuniombea.

## Utangulizi

Mafanikio yanafananishwa na kitu au mnyama mwenye nguvu nyingi na mwenye mbio za kasi kubwa. Kwa upande wa nguvu, mnyama huyo anafananishwa na tembo, farasi au simba. Kwa upande wa mwendokasi, mnyama huyo anafananishwa na mnyama duma.

Ni wazi kuwa wewe una nguvu za kawaida na huwezi kukimbia kwa kasi kubwa sana. Hivyo, mnyama huyo au kitu hicho kimekuzidi nguvu na kimekuzidi mwendokasi pia.

Kwa sababu mnyama huyo amekuzidi kasi ya mbio na nguvu, kuna changamoto hapo. Ili uweze kumkamata mnyama huyo na kumfanya kuwa wako na akakutumikia kwa uaminifu inakuhitaji uwe na maarifa tele na fikra chanya kwenye kila unachokifanya.

Ni jambo jema kutafuta njia ya kummiliki mnyama huyo. Ukimmiliki utaweza kuchuma nguvu zake nyingi na kuzifanya kuwa zako na pia utaweza kuitumia kasi yake kubwa kujiletea maendeleo chanya kwa kasi kubwa; maendeleo yako na jamii inayokuzunguka.

Huko India kuna hadithi moja ambayo husimuliwa juu ya mafunzo ambayo tembo hupitia mpaka kufikia hatua ya kufanywa kuwa mnyama wa kufungwa. Mafunzo hayo huanza kutolewa kwa tembo akiwa bado mtoto. Asipotii, tembo huyo huchapwa sana na kunyimwa chakula. Ili kuziepuka adhabu hizo, tembo hukubali kunyenyekea na kuwa tayari kuongozwa hata na mtoto mdogo.

Tembo huyo hukua katika mazingira hayo akitii maagizo yote kutoka kwa mtu anayemwongoza.

Maamuzi sahihi ya kuchukua ili kuteka mafanikio yako unapaswa uyafanye mapema, kabla umri wako haujaenda sana. Kama nilivyosema hapo juu kuwa mafanikio yako yanafananishwa na

mnyama mwenye nguvu, unapaswa uanze kumfunza mnyama wako utii angali akiwa bado mdogo, akikomaa atakushinda na kukugeuza wewe kuwa mtumwa wake. Ukichelewa utakuwa mtumwa wa mafanikio yako.

Kwenye kitabu hiki tunaenda kujifunza njia mbalimbali zitakazokupa uwezo wa kumteka mnyama huyo na kuweza kumtumia katika harakati zako za kuifanya dunia kuwa sehemu bora zaidi ya kuishi binadamu na viumbe wanaowazunguka.

Mafanikio pia yanafananishwa na kisima chenye kina kirefu nyikani, kisima chenye maji mengi na safi. Ili kupata maji ya kisima hicho na kuyatumia kwa shughuli zetu za kila siku, kunywesha wanyama wetu na kumwagilia mazao yetu yapate kustawi, hatuna budi kujifunza njia nzuri ya kuyateka maji hayo kutoka katika kisima hicho chenye kina kirefu.

Kwenye kitabu hiki tunaenda kujifunza jinsi ya kuyateka maji hayo kwa njia mbalimbali rahisi na kuweza kuyatumia vyema katika kujiletea maendeleo endelevu huko nyikani.

Tunaenda kujifunza jinsi ya kutafuta maarifa yanayohitajika na namna nzuri ya kuyaweka maarifa hayo katika matendo ili yaweze kufanyika kuwa mtego bora wa kuyavutia na kuyanasa mafanikio.

Tunaenda kujifunza jinsi ya kuwa na fikra chanya siku zote tunapoendelea na mchakato wa kuteka mafanikio yetu. Kuna siku mitego yetu itakatwa, kuna siku mitego yetu haitanamata kitu, kuna siku mitego yetu itaonekana haifai kitu; ni jambo jema kutambua la kufanya katika mazingira kama hayo.

Kuna siku moja nikiwa nashawishi kila mmoja wetu, kwenye kikundi chetu cha Upendo, kuwa ajijengee tabia ya kuweka akiba sehemu ya

pato lake kwa ajili ya uwekezaji nilitumia mfumo wa kuuliza maswali.

Maswali yote yalifanana isipokuwa yalitofautiana muda tu. Niliuliza;
Nani ambaye amepanga kufa kesho? Anyoshe mkono.
Nani ambaye amepanga kufa baada ya wiki moja kuanzia sasa?
Nani ambaye amepanga kufa mwezi mmoja kuanzia sasa?
Nani ambaye amepanga kufa mwakani?
Nani ambaye amepanga kufa baada ya miaka 10 kuanzia sasa?
Nani ambaye amepanga kufa baada ya miaka 50 kuanzia sasa?

Kila swali nililoliuliza katika hayo hapo juu hakuna hata mwanakikundi mmoja, katika wanakikundi 25, aliyejitokeza kunyoosha mkono wake kuwa amepanga afe kwenye muda nilioutaja.

Nikawaeleza kuwa, "kumbe kila mmoja wetu hapa amepanga na amechagua kuishi miaka mingi iwezekanavyo hapa duniani."

Sasa kama ni hivyo, kwa nini huchukui hatua ya kuandaa vyema kesho yako? Kwa nini huchukui hatua za makusudi kuboresha mazingira ya dunia yako ambapo ndio makazi yako?

Kwa sababu hutaki kufa leo au kesho, na umechagua kuishi miaka mingi mbeleni unapaswa vilevile uchague kupafanya mahali unapoishi pawe bora zaidi ya ulivyopakuta.

Unapaswa uchukue hatua ya kuboresha mawazo na fikra zako. Ziwe na mlengo chanya. Unapaswa pia kuboresha mawazo na fikra za wanaokuzunguka, maana mawazo yao na fikra zao zina athari kwako ukiamua kuziacha zilivyo.

Kwa maneno mengine ni kwamba, kwa namna yoyote ile sahihi, unapaswa kuwa tayari, kwa moyo mmoja, kuifanya dunia kuwa bora zaidi. Kwamba unapaswa kuifanya kuwa bora maana ni katika dunia hii ndipo utakapoyaishi hayo maisha yako marefu unayoyataka.

Hivyo karibu tujifunze pamoja jinsi ya kufanya maisha yetu na ya dunia kwa ujumla kuwa bora zaidi ya tulivyoyakuta.

**Inawezekana, Timiza Wajibu Wako.**